

## **BURLINGTON REVOLVING LOAN PROGRAMS (MIPANGO YA MIKOPO INAYOPASWA KULIPWA ILI KUKOPESHA TENA YA BURLINGTON)**

Jiji la Burlington limetenga \$500,000 kwa ajili ya fedha za mikopo inayopaswa kulipwa ili kukopesha tena ambazo lengo lake kuu ni kusaidia biashara na viwanda vinavyomilikiwa wa watu wa eneo ambavyo viliathirika au viliathiriwa vibaya na janga la COVID-19, huku likilenga zaidi BIPOC, biashara zinazomilikiwa na wanawake na biashara zingine zisizohudumiwa vya kutosha.

Mipango miwili tofauti ya mikopo inayopaswa kulipwa ili kukopesha tena iliundwa, mmoja kwa ushirikiano na **Kiva kwa mikopo midogo** na mwingine **Burlington Revolving Loan Program (BRLP)**, ili kuzisaidia biashara za Burlington kupata mikopo mikubwa zaidi.

### **Ni mpango gani wa mkopo unaonifaa?**

Ulinganisho ufuatao wa kila kipengee cha mipango hii miwili ya mikopo inayopaswa kulipwa ili kukopesha tena ya Burlington utakusaidia kuamua ni mpango gani unaofaa zaidi mahitaji yako ya biashara, lakini tungependa kukuhimiza uwasiliane na idara ya Business and Workforce Development (BWD, Biashara na Maendeleo ya Wafanyakazi) ili kujadili machaguo zaidi katika [business@burlingtonvt.gov](mailto:business@burlingtonvt.gov).

#### **Mpango wa Kiva Microlending**

Mikopo ya \$1,000 - \$15,000

Kiwango cha Riba cha 0%

Kipindi: Miezi 12-36

Hakuna ada kwa wakopaji

Inazingatia Sheria ya Sharia

#### **Mpango wa Burlington Revolving Loan Program**

Mikopo ya \$10,000 - \$40,000

Kiwango cha Riba cha 0%

Kipindi: Miaka 3-5

Ada ya Kuomba: \$25  
Ada ya usimamizi: 2% ya kiasi  
cha mkopo

Inazingatia Sheria ya Sharia